JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA), 2024

HISABATI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA), 2024

04 HISABATI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania

S.L.P. 2624
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI…………………………………………………………………………iv

1.0 UTANGULIZI 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI ………………………………………………………………………2

2.1 Swali la 1: Kutumia Dhana ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti 3

2.2 Swali la 2: Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku...8

2.3 Swali la 3: Kutumia Stadi ya Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali 12

2.4 Swali la 4: Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati………………………………………………………...18

2.5 Swali la 5: Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali...................... 23

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ULIOPIMWA 28

4.0 HITIMISHO 29

5.0 MAPENDEKEZO 30

Kimbatanisho A: Ufaulu wa Wanafunzi katika Umahiri Uliopimwa katika Upimaji wa SFNA 2024 32

Kimbatanisho B: Ulinganifu wa Ufaulu wa Wanafunzi katika Umahiri Uliopimwa katika Upimaji wa Darasa la Nne SFNA 2024 na 2023.......33

DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2024 kwa somo la Hisabati imeandaliwa ili kuwawezesha wanafunzi, walimu, wakuza mitaala, watunga sera na wadau wengine wa elimu kufahamu jinsi wanafunzi walivyojibu maswali ya Upimaji.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, uchambuzi wa ufaulu, hitimisho na mapendekezo.

Katika taarifa hii, mambo ambayo yalichangia ufaulu wa wanafunzi katika kila swali yameainishwa. Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa mwaka 2024 ufaulu wa wanafunzi ulikuwa wa kiwango kizuri kwa sababu asilimia 71.40 ya wanafunzi 1,530,456 walifaulu upimaji. Mambo yaliyochangia ufaulu wa wanafunzi wengi kuwa mzuri ni uwezo wa kujibu kwa usahihi angalau vipengele vinne kati ya vitano vya kila swali katika umahiri mahsusi uliopimwa.

Hata hivyo, wanafunzi 1,063,514 sawa na asilimia 69.49 walikuwa na ufaulu hafifu katika umahiri mahsusi wa Kutumia Stadi za Uhusiano wa Namba na Vitu Kutatua Matatizo katika Miktadha Mbalimbali. Kiwango hafifu cha ufaulu kilisababishwa na wanafunzi kushindwa kusoma saa na dakika, kujumlisha saa na dakika, kujumlisha fedha za Tanzania, kuzidisha fedha za Tanzania na Kutomudu stadi za Kuandika na Kuhesabu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu katika umahiri mahsusi wa *Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati, Kutumia Dhana ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti* na *Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali*. Hivyo, mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii yatawasaidia wadau wa elimu katika kuboresha na kukuza uwezo wa wanafunzi katika umahiri mahsusi utakaopimwa kwa wakati ujao.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani kwa Maafisa Mitihani pamoja na wataalamu wengine wote kwa ushiriki wao katika kuandaa taarifa hii.

Prof. Said A. Mohamed
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Hisabati ulifanyika tarehe 24 Oktoba, 2024. Jumla ya wanafunzi 1,633,272 walisajiliwa, ambapo kati yao, wanafunzi 1,530,560 sawa na asilimia 93.71 walifanya upimaji wa somo la Hisabati.

Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya upimaji katika somo la Hisabati mwaka 2024 unaonesha kuwa wanafunzi 1,092,786 sawa na asilimia 71.40 walifaulu. Mwaka 2023, wanafunzi 834,119 sawa na asilimia 54.00 walifaulu. Hii inaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kimepanda kwa asilimia 17.40 mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023. Ulinganifu wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika kila Gredi katika Upimaji wa mwaka 2024 na 2023 ni kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na. 1.



Chati Na.1: *Ulinganifu wa Gredi za Wanafunzi katika mwaka 2024 na 2023*

Karatasi ya Upimaji wa somo la Hisabati ilikuwa na jumla ya maswali matano (5). Kila swali lilikuwa na vipengele vitano, ambavyo ni (a), (b), (c), (d) na (e). Jibu sahihi katika kila kipengele lilikuwa na uzito wa alama mbili (02). Hivyo, kila swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na kufanya jumla ya alama 50 katika upimaji wa somo la Hisabati.

Majibu ya wanafunzi kwa kila swali yamechambuliwa ili kubaini sababu zilizofanya wanafunzi kufaulu au kutofaulu Upimaji huo. Sampuli za baadhi ya majibu ya wanafunzi zimewekwa kama vielelezo ili kuonesha uhalisia wa utendaji wa wanafunzi katika swali husika.

Asilimia ya wanafunzi waliofaulu kwa kila swali imetumika kubaini viwango vya ufaulu. Katika uchambuzi, viwango vya ufaulu kwa kila swali vimegawanyika katika makundi manne kama ifuatavyo: alama 10 ni "*kiwango kizuri sana*", 8 ni "*kiwango kizuri*", alama 4 hadi 6 ni "*kiwango cha wastani*" na alama 0 hadi 2 ni "*kiwango hafifu*". Kwa upande mwingine, viwango vya ufaulu kwa kila umahiri uliopimwa vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika umahiri husika ambapo; asilimia 67 - 100 ni *kiwango kizuri cha ufaulu*, asilimia 34 - 66 ni *kiwango cha wastani cha ufaulu* na asilimia 0 - 33 ni *kiwango hafifu cha ufaulu*.

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

Katika taarifa hii, takwimu za ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali au umahiri mahsusi zimewasilishwa kwa kutumia chati. Aidha, rangi za kijani, kijani nyepesi, njano na nyekundu zimetumika

kuonesha viwango vya ufaulu ambavyo ni kiwango "*kizuri sana*", "*kizuri*", "*wastani*" na "*hafifu*" mtawalia.

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kilikuwa kizuri katika swali la 4, 1 na la 5, wastani katika swali la 2 na hafifu katika swali la 3. Katika sehemu hii, kila swali limechambuliwa kwa kuzingatia utendaji wa wanafunzi. Vielelezo vimetumika kuthibitisha hoja zilizotolewa katika kila swali.

2.1 Swali la 1: Kutumia Dhana ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano vilivyopima uwezo wa wanafunzi kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti, kama ifuatavyo**:**

(a)
$$\begin{array}{r} 78 \\ +\ 11 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

(b)
$$\begin{array}{r} 746 \\ +\ 437 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

(c) Andika namba ifuatayo kwa kifupi: 300+60+5 =

(d) Andika 345 kwa kirefu.

(e) Andika XXV kwa namba za Kiarabu.

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi katika: (a) kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kwa wima, (b) kujumlisha namba mbili zenye tarakimu tatu kwa wima, (c) kuandika namba 300

jumlisha 60 jumlisha 5 kwa kifupi, (d) kuandika namba 345 kwa kirefu, (e), Kuandika XXV kwa namba za kiarabu.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 1,209,492 sawa na asilimia 79.02 walipata alama 4 hadi 10. Miongoni mwao wanafunzi 537,342 walipata alama zote 10. Hata hivyo, wanafunzi 321,066 sawa na asilimia 20.98 walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu ambapo 144,330 sawa na asilimia 9.7 hawakupata alama yoyote. Muhtasari wa viwango vya ufaulu kwa swali la 1 umeoneshwa katika Chati Na.2.



Chati Na. 2: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa zaidi ya theluthi moja ya wanafunzi (35.11%) walipata alama zote kumi. Wanafunzi hawa waliweza kutumia dhana ya namba kwa usahihi kuwasiliana katika mazingira tofauti. Katika kipengele (a), waliweza kujumlisha namba zenye tarakimu mbili na kutambua nafasi za tarakimu katika namba na kupata 89. Katika kipengele (b), waliweza kujumlisha namba zenye

tarakimu tatu na kutambua nafasi ya tarakimu katika namba na kupata 1183.

Katika kipengele (c), walijumlisha kwa usahihi 300, 60 na 5 na kupata 365, jibu ambalo ni kifupi cha 300 + 60 + 5. Katika kipengele (d), waliweza kufafanua 345 na kupata 300+40+5. Katika kipengele (e), waliweza kuandika namba 25 baada ya kutambua thamani ya kila herufi iliyotumika kuunda namba ya kirumi, XXV. Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 1 imeoneshwa katika Kielelezo Na. 1.1.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
1. (a)	78 + 11	78 + 11 89	89
(b)	746 + 437	746 + 437 1183	1183
(c)	Andika namba ifuatayo kwa kifupi: 300+60+5 =	300+60+5 = 365	365

(d)	Andika 345 kwa kirefu.	300+40+5=	300+40+5
(e)	Andika XXV kwa namba za Kiarabu.	XXV=25	25

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na.1.1, mwanafunzi alionesha umahiri wa kujibu kwa usahihi kutumia namba kuwasiliana katika mazingira tofauti katika vipengele vyote vya swali.

Kwa upande mwingine, asilimia 20.98 ya wanafunzi walipata alama kuanzia 0 hadi 2, ambao ni ufaulu hafifu. Kiwango hiki cha ufaulu kilitokana na kushindwa kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti. Katika kipengele (a), walikuwa na maarifa kidogo ya kujumlisha namba zenye tarakimu mbili kwa wima. Wanafunzi hawa walijumlisha na kutoa namba zilizotolewa wakati huo huo. Kwa mfano, walijumlisha 78 na 11 na kupata 69 badala ya 89.

Katika kipengele (b), wanafunzi walishindwa kujumlisha namba zenye tarakimu tatu kwa wima kutokana na kukosa stadi ya kuweka tarakimu katika nafasi sahihi ya maelfu, mamia, makumi na mamoja. Hivyo, wengi walishindwa kuweka fungu 1 la maelfu lililozidi katika mamia katika maelfu. Kwa mfano, wanafunzi wengi walijibu swali 746+487 kwa kuandika majibu yasiyo sahihi kama vile 183, 283 na 1831.

Katika kipengele (c), baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha dhana ya kuandika namba kwa kifupi na kwa maneno. Kwa mfano, mwanafunzi aliandika 300 + 60 + 5 ni sawa na elfu tatu sitini na tano badala ya 365. Wanafunzi wengine waliunganisha 300, 60 na 5 kienyeji bila kufuata taratibu za namba tatu kwa ulalo na kupata 300605.

Katika kipengele (d), walishindwa kujumlisha 300, 40 na 5 ili kufafanua 345 katika 300+40+5. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliongeza 0 kwa 300 na 40 na kupata 345=3000+400+5. Katika kipengele (e), walishindwa kujumlisha thamani ya kila herufi katika XXV ili kupata 25. Kwa mfano, wanafunzi kadhaa waliunganisha thamani ya kila herufi katika XXV na kupata 10,105 badala ya 25. Sampuli ya sehemu ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa wanafunzi waliojibu swali la 1 imeoneshwa katika Kielelezo Na. 1.2.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(d)	Andika 345 kwa kirefu.	3 4 5	34+45+5+
(e)	Andika XXV kwa namba za Kiarabu.	X X4	1015

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Kielelezo Na.1.2 kinaonesha majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi aliyeshindwa kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti. Katika kipengele (d), mwanafunzi alishindwa kuweka 3, 4 na 5 katika nafasi ya maelfu, mamia na mamoja

mtawalia. Aidha, katika kipengele (e), mwanafunzi alishindwa kuandika XXV kwa kiarabu kwa kutotambua nafasi ya kila tarakimu katika namba za kirumi.

2.2 Swali la 2: Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano ambavyo vilipima uwezo wa wanafunzi katika kutumia stadi za mpangilio katika maisha ya kila siku. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

(a) Andika namba inayofuata katika mpangilio wa namba zifuatazo: 1, 3, 5, 7, ___________.

(b) Panga namba zifuatazo kuanzia ndogo hadi kubwa zaidi: 23, 12, 34, 21, 32, 43, 18.

(c) Andika namba ambayo inayokosekana katika mpangilio wa namba za Kirumi ufuatao: XII, XIV, XVI, ____, XX.

(d) Jaza namba inayokosekana katika mpangilio wa namba ufuatao: 998, 999, 1000, ___.

(e) Kijiji cha Nguvumali kilivuna mahindi kwa miaka 5. Kila mwaka yaliongezeka magunia 50. Iwapo mwaka wa kwanza walivuna magunia 300, je mwaka wa 5 walivuna magunia mangapi?

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi katika: (a) kubaini namba inayokosekana katika mpangilio wa namba zinazoongezeka kwa 2, (b) Kupanga namba kuanzia ndogo hadi kubwa zaidi. (c) Kuandika namba ambayo inakosekana katika mpangilio wa namba za kirumi. (d) Kujaza namba inayokosekana katika mpangilio wa namba

zinazopungua kwa 1 na (e) kufumbua fumbo linalohusu mpangilio wa namba unaongezeka kwa 50.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 1,530,558 walijibu swali hili. Kati ya hao, wanafunzi 627,924 sawa na asilimia 41.02 walipata alama 0 hadi 2, wanafunzi 578,878 sawa na asilimia 37.83 walipata alama 4 hadi 6, wanafunzi 261,953 sawa na asilimia 17.11 walipata alama 8 wakati wanafunzi 61,803 sawa na asilimia 4.04 walipata alama 10. Katika swali hili, kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa ujumla kilikuwa kizuri kwa sababu asilimia 79.02 ya wanafunzi walipata alama 4 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 2.



Chati Na. 3: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Katika kipengele (a), waliweza kubaini kuwa namba zilizopo katika mpangilio wa namba uliotolewa zinaachana kwa 2. Hivyo, walijumlisha 7 na 2 na kupata jibu sahihi ambalo ni 9. Katika kipengele (b), walipanga namba katika mfululizo wa namba kuanzia ndogo hadi kubwa na kupata 12, 18, 21, 23, 32, 34, 43. Katika kipengele (c), Waliweza kubaini kuwa

namba ambayo inakosekana katika mpangilio wa namba za kirumi uliotolewa ni XVIII.

Katika kipengele (d), waliweza kubaini kuwa namba katika mpangilio 998, 99, 1000, ___ zinaachana kwa 1. Kwa hiyo, walijumlisha 1000 na 1 na kupata 1001. Katika kipengele (e), waliweza kutumia taarifa zilizopo kwenye fumbo la mpangilio wa namba uliotolewa kuunda mpangilio 300, 350, 400, 450, 500. Kisha walibaini kuwa mwaka wa 5, wanakijiji cha Nguvumali walivuna magunia 500. Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 2 imeoneshwa katika Kielelezo Na. 2.1.

2.(a)	Andika namba inayofuata katika mpangilio wa namba zifuatazo: 1, 3, 5, 7, ____________.	1, 3, 5, 7, 9	Namba inayokosekana ni 9
(b)	Panga namba zifuatazo kuanzia ndogo hadi kubwa zaidi: 23, 12, 34, 21, 32, 43, 18.	23, 12, 34, 21, 32, 43, 18 12, 18, 21, 23, 32, 34, 43.	12, 18, 21, 23, 32, 34, 43.
(c)	Andika namba ambayo inakosekana katika mpangilio wa namba za Kirumi ufuatao: XII, XIV, XVI, ____, XX.	XII, XIV, XVI, XVIII, XX.	Namba inayokosekana ni XVIII
(d)	Jaza namba inayokosekana katika mpangilio wa namba ufuatao: 998, 999, 1000, 1001.	998, 999, 1000, 1001.	Namba inayokosekana ni 1001
(e)	Kijiji cha Nguvumali kilivuna mahindi kwa miaka 5. Kila mwaka yaliongezeka magunia 50. Iwapo mwaka wa kwanza walivuna magunia 300, je mwaka wa 5 walivuna magunia mangapi?	300 + 50 = 350 350 + 50 = 400 400 + 50 = 450 450 + 50 = 500	Mwaka wa tano walivuna magunia 500

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.1, mwanafunzi aliandika majibu sahihi katika vipengele vyote vya swali hili.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 378,953 sawa na asilimia 24.76 hawakupata alama yoyote. Katika kipengele (a), walishindwa kubaini kuwa namba katika mfululizo uliotolewa ni namba witiri. Kwa mfano, wanafunzi kadhaa waliandika kuwa namba inayokosekana ni 8. Wanafunzi waliunganisha 9 na 11 na kuandika 911. Katika kipengele (b), wanafunzi wengi walipanga namba zilizotolewa kuanzia kubwa kwenda ndogo ambapo waliandika 43, 34, 23, 21, 18, 12 badala ya 12, 18, 21, 23, 32, 34, 43. Katika kipengele (c), walishindwa kubaini namba ya kirumi inayokosekana katika mpangilio wa namba za kirumi zilizotolewa. Kwa mfano, wanafunzi wengi waliunganisha I na namba ya Kirumi kabla ya nafasi iliyoachwa wazi na kupata XVII. Wengine waliandika namba inayokosekana kwa namba za Kiarabu (18) kinyume na matakwa ya swali. Katika kipengele (d), wanafunzi wengi waliunganisha 1000 na 1 kienyeji na kupata 10001. Katika kipengele (e), wanafunzi wengi walizidisha 300 na 50 na kupata 15000 badala ya 500. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sehemu ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa wanafunzi waliojibu swali la 2.

(d)	Jaza namba inayokosekana katika mpangilio wa namba ufuatao: 998, 999, 1000, ___.	998, 999, 1000	10001
(e)	Kijiji cha Nguvumali kilivuna mahindi kwa miaka 5. Kila mwaka yaliongezeka magunia 50. Iwapo mwaka wa kwanza walivuna magunia 300, je mwaka wa 5 walivuna magunia mangapi?	+ 50 5 + 50 5 +355	355

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2, mwanafunzi alishindwa kujumlisha namba katika mfuatano wa namba uliotolewa katika kipengele (d). Aidha katika kipengele (e), alishindwa kubaini matakwa ya swali.

2.3 Swali la 3: Kutumia Stadi ya Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano vilivyopima uwezo wa wanafunzi katika kutumia stadi za uhusiano wa namba na vitu kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali. Swali liliuliza kama ifuatavyo:

(a) Jumlisha; sh. 2150 + sh. 950 =.

(b) Zidisha;

$$\begin{array}{r} \text{Sh. } 250 \\ \times \quad 30 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

(c) Andika muda uliooneshwa kwenye saa kwa maneno.



(d) Andika Saa mbili kasoro robo kwa namba.

(e)

	saa	dakika
	4	30
	+2	45

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi katika: (a) kujumlisha fedha kwa ulalo, (b) kuzidisha fedha na namba kwa wima, (c) kuandika wakati kwa kutumia mchoro wa saa, (d) Kuandika muda uliotolewa kwa namba na (e) kujumlisha vipimo vya wakati.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 1,530,558 walifanya swali hili. Wanafunzi 1,063,514 ambao ni sawa na asilimia 69.49. walipata alama 0 hadi 2 ambapo wanafunzi 715,936 ambao ni sawa na asilimia 46.78 walipata alama 0. Wanafunzi 336,588 sawa na asilimia 21.99 walipata alama 4 hadi 6 na wanafunzi 45,742 sawa na asilimia 2.99 walipata alama 10. Chati. Na. 4 inaonesha ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika Swali la 3.



Chati Na. 4: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Kama inavyoonekana katika Chati. Na. 4, wanafunzi wengi walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Wanafunzi hao walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kushindwa kutumia matendo ya namba ya kihisabati kutatua matatizo. Katika kipengele (a), walishindwa kujumlisha fedha iliyotolewa. Kwa mfano, wanafunzi wengi walijumlisha sh. 2,150 na sh. 950 na kupata sh. 2,100 badala ya sh. 3,100. Katika kipengele (b), walishindwa kuzidisha fedha kwa namba yenye tarakimu mbili. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alizidisha sh. 250 kwa 30 na kupata 280. Aidha, mwingine alipata 80 badala ya sh. 7,500.

Katika kipengele (c), walishindwa kusoma muda uliooneshwa kwenye mchoro wa saa waliopewa. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina ya mishale na nadharia ya mshale wenye kuonesha dakika na wenye kuonesha saa. Kwa mfano, wanafunzi kadhaa waliandika saa mbili na dakika tatu, wengine waliandika saa nane tatu, wakati wengine waliandika saa

tatu na dakika nane badala ya saa nane na dakika kumi na tano. Wengine walitumia mshale wa saa kwa dakika na mshale wa dakika kwa saa na hivyo kuandika saa tisa na dakika nane badala ya saa nane na dakika kumi na tano. Katika kipengele (d), walishindwa kuandika muda uliotolewa kwa namba. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika 2:45 badala ya kuandika 1:45. Katika kipengele (e), walishindwa kujumlisha saa na dakika kwa usahihi. Kwa mfano, wanafunzi wengi walishindwa kuhamisha saa moja iliyozidi upande wa dakika kwenda upande wa saa na hivyo kuandika 75 badala ya 15. Sampuli ya majibu yasiyo sahihi inaoneshwa katika kielelezo Na. 3.1.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(c)	Andika muda uliooneshwa kwenye saa kwa maneno. 	Saa tatu na dakika nane	Saa tatu na dakika nane
(d)	Andika Saa mbili kasoro robo kwa namba.	2.00	2.00
(e)	saa dakika 4 30 +2 45	6.75	6.00

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

Katika kielelezo Na. 3.1, mwanafunzi alishindwa kubaini kubaini, uliooneshwa kwenye uso wa saa. Katika kipengele (d), mwanafunzi alishindwa kuandika muda uliotolewa kwa namba. Katika kipengele (e), mwanafunzi alishindwa kutambua uhusiano wa saa na dakika kuwa saa 1 ni sawa na dakika 60.

Licha ya kiwango hafifu cha ufaulu wa wanafunzi, wanafunzi 45,742 (2.99%) walipata alama zote 10. Wanafunzi hawa waliweza kujumlisha sh.2150 na sh.950 na kupata sh. 3100 katika kipengele (a). Katika kipengele (b), waliweza kuzidisha kwa usahihi fedha (sh.250) kwa namba yenye tarakimu mbili (30) na kupata sh. 7500. Katika kipengele (c), waliweza kubaini kuwa mshale mfupi hutumika kusoma saa na mshale mrefu hutumika kusoma dakika, hivyo waliandika kwa usahihi muda uliooneshwa kwenye saa kwa maneno "saa mbili na robo". Katika kipengele (d), waliweza kuandika kwa usahihi kuwa saa mbili kasoro robo katika namba ni 1: 45. Katika kipengele (e), waliweza kujumlisha saa na dakika kwa usahihi. Aidha, waliweza kuhamisha saa 1 iliyozidi kutoka upande dakika kwenda upande wa saa 75. Hivyo, walipata jumla ya saa na dakika zilizotolewa kuwa ni saa 7 dakika 15. Sampuli ya majibu sahihi imeoneshwa katika kielelezo Na. 3.2.

3. (a)	Jumlisha; sh. 2150 + sh. 950 =	2150 +950 3100	Sh. 3100
(b)	Zidisha; Sh. 250 x 30	250 X 30 000 +750 7500	Sh. 7500
(c)	Andika muda uliooneshwa kwenye saa kwa maneno. 	8: 15	Saa 8: 15 Saa nane na robo
(d)	Andika Saa mbili kasoro robo kwa namba.	1: 45	saa 1: 45
(e)	saa dakika 4 30 +2 45	4 30 +2 45 6 75 60	Saa 7 dk 15

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu sahihi kwa Swali la 3

Katika Kielelezo Na. 3.2, mwanafunzi aliweza kujumlisha na kuzidisha fedha kwa usahihi katika kipengle (a) na (b). Katika kipengele (c), mwanafunzi aliandika kwa usahihi muda uliotolewa kwenye saa kwa maneno. Katika kipengele (d), mwanafunzi aliandika muda uliotolewa kwa maneno katika namba. Katika kipengle (e), mwanafunzi aliweza kujumlisha kwa usahihi dakika na saa zilizotolewa.

2.4 Swali la 4: Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati

Swali la 4 lilitoka katika umahiri mahsusi wa kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya hisabati na lilikuwa na vipengele vitano kama ifuatavyo:

(a) Umbo la mraba lina pembe ngapi?

(b) Chora umbo lenye pembe tatu.

(c) Tafuta mzingo wa mraba ufuatao:



(d) Chumba cha zahanati kina umbo la mstatili wenye mzingo wa m 54. Ikiwa urefu wake ni m 17, tafuta upana wa chumba hicho.

(e) Mzingo wa pembetatu ni sm 70. Ikiwa upande wa kwanza una urefu wa sm 24 na upande wa pili sm 25, tafuta urefu wa upande wa tatu.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi katika kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya kihisabati kama ifuatavyo: (a) kutaja jumla ya pembe katika umbo la mraba, (b) kuweza kuchora umbo lenye pembe tatu, (c) kutafuta mzingo wa mraba, (d) kufumbua fumbo linalohusu mzingo wa mstatili na (e) kufumbua fumbo linalohusu mzingo wa pembetatu.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 1,591,702 walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 1,240,275 sawa na asilimia 81.03 walipata alama 4 hadi 10 na hivyo kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Hata hivyo, wanafunzi 290,083 (18.97%) walikuwa na ufaulu hafifu katika swali hili kwa kupata alama kati ya 0 hadi 2. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4 umeoneshwa katika chati Na. 5.



Chati Na. 5: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4*

Wanafunzi 59,393 sawa na asilimia 3.88 waliopata alama zote walielewa kuwa umbo la mraba lina pembe nne katika kipengele (a). Katika kipengele (b), waliweza kuchora umbo lenye pembe tatu. Katika kipengele (c), waliweza kutafuta kwa usahihi mzingo wa mraba wenye urefu wa m 14 na kupata sm 56. Katika kipengele (d), waliweza kufumbua fumbo lililotolewa kwa usahihi ambapo walitumia kanuni ya kukokotoa mzingo wa mstatili ambayo ni mzingo = (urefu + upana) x 2 na kupata m 10 ambao ni urefu wa mstatili huo. Katika kipengele (e), waliweza kutumia

mzingo wa pembe uliotolewa ambao ni sm 70, urefu wa upande wa kwanza (sm 24) na wa pili (sm 25) pamoja na kanuni ya kutafuta mzingo (mzingo wa pembetatu = urefu + urefu + urefu). Vilevile, walikokotoa kwa usahihi na sm 21 za upande wa tatu wa pembetatu. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 4.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
4 .(a)	Umbo la mraba lina pembe ngapi?	pembe 4	pembe4
(b)	Chora umbo lenye pembe tatu.		
(c)	Tafuta mzingo wa mraba ufuatao: sm 14 	up x 4 sm14 x 4 = sm56	sm56
(d)	Chumba cha zahanati kina umbo la mstatili wenye mzingo wa m 54. Ikiwa urefu wake ni m 17, tafuta upana wa chumba hicho.	(ur)+(up) x 2 54 = (17 + up) x 2 54 = 34 + 2up 54 - 34 = 2up 20/2 = 2up/2 up = 10 up = sm10	sm10
(e)	Mzingo wa pembetatu ni sm 70. Ikiwa upande wa kwanza una urefu wa sm 24 na upande wa pili sm 25, tafuta urefu wa upande wa tatu.	70 = 24+25+ur 70 = 49 + ur ur = 70-49 ur = 21	sm21

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya mjibu sahihi kwa Swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.1, mwanafunzi alikuwa na ujuzi wa kutosha katika aina mbalimbali za maumbo katika vipengele (a) na (b). Katika vipengele (c), (d), na (e), mwanafunzi alikuwa mahiri katika kutumia kanuni za kukokotoa mzingo wa maumbo mbalimbali, kama vile mraba, mstatili na pembetatu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 141,976 sawa na asilimia 9.28 walishindwa kupata alama yoyote. Katika kipengele (a), walishindwa kutaja idadi ya pembe katika umbo la mraba. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alichora pembetatu na kuandika kuwa jibu ni tatu. Mwanafunzi mwingine alichora umbo la pembe tatu pacha. Katika kipengele (b), walishindwa kuchora umbo lenye pembe tatu. Kwa mfano, wanafunzi kadhaa waliandka 3 na wengine waliandika aina za maumbo kama vile mraba, mstatili na pembe tatu.

Katika kipengele (c), walishindwa kukumbuka kanuni ya kutafuta mzingo wa mraba. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alizidisha urefu wa upande mmoja wenye sm 14 kwa 2 na kupata sm 28 badala ya sm 56. Mwanafunzi mwingine alijumlisha pande nne za mraba na kupata sm 30 badala ya sm 56.

Katika kipengele (d), walishindwa kufumbua fumbo lenye kuhitaji matumizi ya kanuni ya mzingo wa mstatili. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walijumlisha mzingo na urefu wa umbo na kupata m 71. Wanafunzi wengine walikokotoa tofauti ya mzingo na urefu wa mstatili na kupata m 37. Wanafunzi wengine walikuwa na uelewa wa kanuni ya mzingo wa mstatili kuwa ni; (urefu + upana) x 2 lakini mzingo wa mstatili waliuchukulia kama urefu na urefu waliuchukulia kama upana yaani (54 + 17) x 2 = 142.

Katika kipengele (e), walishindwa kutumia mzingo wa pembetatu kukokotoa urefu wa upande wa tatu. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walichora pembetatu na kuandika tarakimu walizopewa kwenye pande tatu za pembetatu kuwa ni 24, 25 na 70 badala ya sm 21. Wanafunzi wengine walidhani kuwa urefu wa pande za pembetatu unatofuatiana kwa sm 1 hivyo walijumlisha sm 25 na sm 1 na kupata sm 26 kama urefu wa upande wa tatu. Wanafunzi wengine waliweza kukumbuka kwa usahihi kanuni ya mzingo wa pembetatu (a + b + c), lakini walichukulia mzingo kama sehemu ya urefu wa pembetatu. Hivyo, walijumlisha 70, 24 na 25 na kupata sm 119. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sehemu ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa wanafunzi waliojibu swali la 4.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(c)	Tafuta mzingo wa mraba ufuatao: sm 14	14 +14 28 28 46	sm=46
(d)	Chumba cha zahanati kina umbo la mstatili wenye mzingo wa m 54. Ikiwa urefu wake ni m 17, tafuta upana wa chumba hicho.	54 +17 71	m=21

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa Swali la 4

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha kuwa mwanafunzi alishindwa kutumia stadi za maumbo katika miktadha ya kihisabati. Katika kipengele (c), mwanafunzi alikosea kujumlisha pande nne za mraba na kupata 46 badala ya 56. Katika kipengele (d),

mwanafunzi alijumlisha mzingo na upande aliopewa badala ya kutumia kanuni ya kutafuta mzingo wa mstatili ili kupata upana.

2.5 Swali la 5: Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano ambavyo vilipima uwezo wa wanafunzi katika kutumia dhana ya stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali. Swali liliuliza kama ifuatavyo:

Tumia takwimu kwa picha kujibu maswali yafuatayo:



(a) Je, mwaka 2011 ilipandwa miti mingapi?
(b) Mwaka upi ilipandwa miti michache zaidi?
(c) Kuna tofauti ya miti mingapi kati ya iliyopandwa 2011 na 2012 ?
(d) Mwaka upi ilipandwa miti mingi zaidi?
(e) Je, jumla ya miti mingapi ilipandwa kwa miaka yote mitatu?

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi katika: (a) kutafuta jumla ya miti iliyopandwa mwaka 2011, (b) kutambua ni mwaka upi ilipandwa miti michache zaidi, (c) kutafuta tofauti ya miti iliyopandwa mwaka 2011 na 2012, (d) kubaini mwaka ambao ilipandwa miti mingi zaidi na (e) kutafuta jumla ya miti iliyopandwa kwa miaka yote mitatu.

Uchambuzi uliofanywa unaonesha kwamba wanafunzi 378,749 sawa na asilimia 24.75 walipata alama 0 hadi 2; wanafunzi 395,607 sawa na asilimia 28.15 walipata alama 4 hadi 6; wanafunzi 471,140 sawa na asilimia 28.48 walipata alama 8 na wanafunzi 285,062 sawa na asilimia 18.62 walipata alama kumi kamili. Kwa jumla, wanafunzi walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani wanafunzi 1,151,809 sawa na asimilia 75.25 walipata alama 4 hadi 10. Chati Na.6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika Swali la 5.



Chati Na. 6: *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa asilimia 18.62 ya wanafunzi waliojibu swali hili waliandika majibu sahihi. Katika kipengele (a), waliweza kuhesabu kwa usahihi idadi ya miti iliyopandwa mwaka 2011 na kupata 14. Katika kipengele (b), waliweza kubaini kuwa mwaka 2012 ndio mwaka ambao ilipandwa miti michache zaidi. Katika kipengele (c), waliweza kuhesabu miti iliyopandwa mwaka 2011 na 2012 na kupata 14 na 8 mtawalia. Kisha walitoa 8 kutoka kwenye 14 na kupata 6 ambayo ni tofauti ya miti iliyopandwa 2011 na 2012. Katika kipengele (d), waliweza kubaini kuwa mwaka 2012 ndio mwaka ambao ilipandwa miti mingi zaidi. Katika kipengele (e), waliweza kujumlisha kwa usahihi 14, 8 na 11 ambayo ni miti iliyopandwa mwaka 2011, 2012 na 2013 mtawalia na kupata kuwa jumla ya miti iliyopandwa miaka yote mitatu ni 33. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo kati ya waliojibu swali la 5.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(a)	Je, mwaka 2011 ilipandwa miti mingapi?	Mwaka 2011 ilipandwa miti 14	Mwaka 2011 ilipandwa miti 14
(b)	Mwaka upi ilipandwa miti michache zaidi?	Mwaka 2012 Mwaka uliopandwa miti michache zaidi ni mwaka 2012	Mwaka ulio pandwa miti michache zaidi ni Mwaka 2012
(c)	Kuna tofauti ya miti mingapi kati ya iliyopandwa 2011 na 2012 ?	2011 miti 14 2012 miti 8 6 Tofauti ni miti 6	Tofauti yake ni miti 6
(d)	Mwaka upi ilipandwa miti mingi zaidi?	Mwaka uliopandwa miti mingi zaidi ni mwaka 2011	Mwaka ulio pandwa miti mingi zaidi ni mwaka 2011
(e)	Je, jumla ya miti mingapi ilipandwa kwa miaka yote mitatu?	miti 14 miti 11 miti 8 miti 33 Jumla ya miti 33	Jumla ya miti 33

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5

Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha kwamba mwanafunzi alitumia kwa usahihi picha zinazowakilisha idadi ya miti iliyopandwa mwaka 2011, 2012, na 2013, na pia alitoa majibu sahihi kwa vipengele vyote vitano vya Swali la 5.

Licha ya ufaulu mzuri wa wanafunzi, walikuwepo wanafunzi 288,813 sawa na asilimia 18.62 ambao hawakupata alama yoyote. Katika kipengele (a), walishindwa kuhesabu idadi ya miti iliyopandwa mwaka 2011. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika mti mmoja. Katika kipengele (b), walishindwa kufanya

uchambuzi wa idadi ya miti iliyopandwa mwaka 2011, 2012 na 2013 na kisha kubaini mwaka ambao ilipandwa miti michache.

Katika kipengele (c), walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, idadi kubwa ya wanafunzi walijumlisha miaka iliyotajwa na kupata 4023 badala ya miti 8. Aidha, wengine walijumlisha mwaka 2011 na 2012 na kupata 4023. Katika kipengele (d), walishindwa kutambua mwaka ambao miti ilipandwa mingi zaidi. Wengi waliandika 14 ambayo ni miti iliyopandwa badala ya mwaka 2011. Aidha, wengine walijibu tofauti na matakwa ya swali. Kwa mfano mwanafunzi mmoja aliandika alhamisi na jumamosi. Katika kipengele (e), walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano idadi kubwa ya wanafunzi walijumlisha mwaka 2011, 2012 na 2013 na kupata 6036 badala ya kutafuta jumla ya picha kwa miaka yote. Sampuli ya majibu yasiyo sahihi imeoneshwa kaitka Kielelezo Na. 5.2.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(a)	Je, mwaka 2011 ilipandwa miti mingapi?	2011	11
(b)	Mwaka upi ilipandwa miti michache zaidi?	mwakaupiilipandwamiti michache	Jumaine
(c)	Kuna tofauti ya miti mingapi kati ya iliyopandwa 2011 na 2012 ?	2012 2011	Jumatatu
(d)	Mwaka upi ilipandwa miti mingi zaidi?	mingi zaidi	Jumatatu
(e)	Je, jumla ya miti mingapi ilipandwa kwa miaka yote mitatu?	miakayote	mitatu

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya mjibu yasiyo sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha kuwa katika kipengele (a), mwanafunzi alipata miti 11 badala ya miti 14. Katika kipengele (b), mwanafunzi alishindwa kuelewa matakwa ya swali. Aidha, aliandika jumanne badala ya mwaka 2012. Katika kipengele (c), mwanafunzi aliandika jumatatu badala miti 6. Katika kipengele (d), mwanafunzi aliandika jumatatu badala ya mwaka 2011. Katika kipengele (e), mwanafunzi aliandika miti mitatu badala ya 33.

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ULIOPIMWA

Karatasi ya Upimaji wa somo la Hisabati ilikuwa na maswali matano (05) ambayo yalipima umahiri mahsusi *wa Kutumia Dhana*

ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti, Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku, Kutumia Stadi ya Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali, Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati na *Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali*.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa umahiri mahsusi tatu (03) zilizopimwa zilikuwa na ufaulu mzuri, umahiri mahsusi mmoja (01) wa *Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku* ulikuwa na ufaulu wa wastani na umahiri mahsusi wa *Kutumia Stadi ya Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali* ulikuwa na ufaulu hafifu. Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2024 na 2023, unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika umahiri mahsusi wa *Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati, Kutumia Dhana ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti, Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali, Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku* na *Kutumia Stadi ya Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali* kilipanda kwa asilimia 62.90, 22.88, 13.16, 35.74 na 9.54 mtawalia. (Ona kiambatanisho A na B).

4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya upimaji katika somo la Hisabati mwaka 2024 unaonesha kuwa wanafunzi 1,092,786 sawa na asilimia 71.40 walifaulu kwa kupata Gredi A hadi D. Aidha, ufaulu wa jumla katika umahiri mkuu wa aina tatu uliopimwa ulikuwa kama ifuatavyo: Kutumia lugha ya Kihisabati Kuwasilisha Wazo au Hoja katika Maisha ya Kila Siku (77.14%), Kufikiri na

Kuhakiki katika Maisha ya Kila Siku (70.00%) na Kutatua Matatizo katika Mazingira Tofauti (30.51%).

Hata hivyo, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu katika kila umahiri mahsusi uliopimwa unaonesha kuwa umahiri wa Kutumia Stadi za Maumbo katika Miktadha ya Hisabati, Kutumia Dhana ya Namba Kuwasiliana katika Mazingira Tofauti na Kutumia Stadi za Takwimu Kuwasilisha Taarifa Mbalimbali ulikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 81.03, 79.02 na 75.25 mtawalia. Aidha, wanafunzi walikuwa na ufaulu wa wastani katika umahiri mahsusi wa Kutumia Stadi za Mpangilio katika Maisha ya kila Siku (58.98%). Hata hivyo, walikuwa na ufaulu hafifu katika umahiri mahsusi wa Kutumia Stadi za Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali (30.51%).

Kiwango hafifu cha ufaulu katika umahiri mahsusi wa Kutumia Stadi za Uhusiano wa Namba na Vitu katika Miktadha Mbalimbali kilitokana na wanafunzi kushindwa kusoma saa na dakika, kujumlisha saa na dakika, kujumlisha fedha, kushindwa kuzidisha fedha na Kutomudu stadi za Kuandika na Kuhesabu.

5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha utendaji wa wanafunzi wa Darasa la Nne katika mahsusi ambazo ufaulu wake ulikuwa hafifu, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Kwa kutumia michoro na saa, walimu waoneshe uhusiano uliopo kati ya saa na dakika na wasisitizwe kuzingatia uhusiano huo wakati wa kujumlisha na kutoa saa na dakika.

(b) Wanafunzi washirikishwe kwenye michezo inayohusiana na kusoma saa ili kubainisha nyakati mbalimbali kwa maneno na kwa tarakimu.

(c) Wanafunzi wahimizwe kutumia saa za kawaida zenye mshale mfupi na mshale mrefu ili waweze kusoma wakati kwa usahihi kama vile saa moja kamili, saa moja na nusu, saa moja kasorobo n.k.

Kimbatanisho A: **Ufaulu wa Wanafunzi katika Umahiri Uliopimwa katika Upimaji wa SFNA 2024**



Kimbatanisho B: **Ulinganifu wa Ufaulu wa Wanafunzi katika Umahiri Uliopimwa katika Upimaji wa Darasa la Nne SFNA 2024 na 2023**